# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Dodoma***
***17 Januari, 2025***

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uhamisho na uteuzi wa viongozi mbalimbali. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka, uhamisho na uteuzi huo ni kama ifuatavyo:

(i) Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe amehamishwa kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwenda kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya;

(ii) Dkt. John Anthony Jingu amehamishwa kutoka Wizara ya Afya kwenda kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; na

(iii) Dkt. Grace Elias Magembe ameteuliwa kuwa Mganga Mkuu wa Serikali. Kabla ya uteuzi huu Dkt. Magembe alikuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, anachukua nafasi ya Prof. Tumaini Joseph Nagu ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Uhamisho na uteuzi huu unaanza mara moja.

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu